

Jukwaa la Kutunga Sheria ya Ulemavu wa Ucheleweshaji wa Kukua ya Kaunti ya King

Huduma kwa watu walio na ucheleweshaji wa kukua na ulemavu wa kiakili na/au kukua (I/DD) zinapaswa kuwa endelevu na kukuza usawa, ushirikishwaji, na ujumuishaji. Vipaumbele hivi vinaweza kuendeleza maono hayo. Huakisi maoni kutoka kwa jumuiya zilizoathiriwa kote katika Kaunti ya King, zikizingatia watu walio na ucheleweshaji na ulemvu wa kiakili na kukua, na Weusi, Wenyeji na Watu wa Rangi. Kaunti ya King inahimiza bunge kushughulikia viptaumbele hivi mwaka wa 2025:



VIPAUMBELE VYA KISHERIA



Ufikiaji wa Lugha

Kukuza ufikiaji wa lugha kwa watoto wote na watu binafsi walio na ulemavu wa akili na ukuaji (I/DD) kwa kutoa ufadhili kwa watoa huduma ya usaidizi wa lugha ya kuzungumza na ishara.



Ufadhilli wa Elimu Maalum

Kuboresha ufikiaji wa usaidizi wa mapema kwa watoto wachanga na watoto wadogo (ESIT) wenge umri wa miaka 0-3 kwa kupanga upya sera za ufadhilli ili kuhakikisha kwamba viwango vya ufadhilli wa elimu maalum ya umri wa miaka 0-3 vinaongezwa ili kulingana na viwango vya umri wa miaka 3-5 na kuongezeka wakati wowote viwango vinaongezeka kwa umri wa miaka 3-5.



Hali ya Kitabia

Kuimarisha huduma na matibabu kwa vijana walio na matatizo ya afya ya kitabia na I/DD walio katika hali mbaya kwa kuendeleza na kupanua timu za usaidizi wa afya ya kitabia na kukuza uwezo wa matibabu ya makazi ya muda mfupi kwa vijana.



Mpito wa Shule

Kudumisha ufikiaji wa uwekezaji wa mpito wa shule ya upili kwa wanafunzi walio na I/DD kwa kuendelea kutoa ufadhilli ili kusaidia katika ajira na huduma zingine muhimu.



Ajira na Ushirikishwaji

Kulinda fursa za ajira na ushirikishwaji wa maana katika jamii kuititia kuongeza malipo ya watoa huduma ili kuimarisha wafanyakazi ambaao wangesaidia kuepuka ucheleweshaji au ukatizaji katika upatikanaji wa huduma.



Makazi

Kuongeza na kudumisha ufikiaji wa nyumba za bei nafuu na huduma za jumla. Kuwekeza katika Hazina ya Dhamana ya Makazi, ikijumuisha ufadhilli wa ukarabati, na kuongeza ufadhilli wa uendeshaji na huduma za usaidizi wa makazi.



Ajenda

6:00 PM	Milango Inafunguliwa <ul style="list-style-type: none"> • Jukwaa: Ukumbi wa Densi • Chumba cha familia: Chumba cha Paradiso (kutazama jukwaa ukiwa mbali) • Chumba cha Utulivu: Chumba cha Bodi ya Vashon, ghorofa ya 2 (hakuna chaguo la kutazama jukwaa)
6:15 PM	Mikutano ya Mapokezi ya Umma na Mazungumzo
7:00 PM	Jukwaa la Kutunga Sheria: Ukaribisho na Hotuba ya Ufunguzi <ul style="list-style-type: none"> • Emcee mweza: Ros Damm, Vice President, King County Champions Chapter of People First of Washington and Eric Matthes, Community Advocacy Coordinator, The Arc of King County • Co-Hosts: Magan Cromar, Mkurugenzi wa Idara, and Holly Woo, Naibu Mkurugenzi wa Idara, Idara ya Ulemavu wa Kukua na Msaada wa Utotoni (DDECSD) • Utambuaji wa Ardhi ya Asili, Katherine Festa, Haida Tribe, DDECSD • Shannon Braddock, Naibu Mtendaji Mkuu wa Kaunti ya King • Haki ya Ulemavu na Usawa wa Kikabila: Adana Protonentis, Co-Owner & Learning Inciter, Kindred Consulting
7:20 PM	Vipaumbele vya Sheria vya 2025 na Wazungumzaji wa Jumuiya
8:00 PM	Utambulisho na mawazo ya wabunge
8:30 PM	Hotuba ya Kufunga



Tafuta wilaya yako ya kutunga sheria



Shiriki maoni yako

*Kwa maelezo zaidi kuhusu vipaumbele vya kisheria, tafadhali wasiliana na:
 Joe McDermott, State Relations Director, jmcdermott@kingcounty.gov or (206) 477-3917.*